# Yaliyomo

**Yaliyomo ......................................................................1**

**Utangulizi ....................................................................3**

**Utangulizi wa mfasiri ....................................................5**

**Asili ia madhehebu yao..................................................7**

**Itikadi zao kwa Allah......................................................7**

**Kauli yao kuhusu kupotoshwa kwa Qur'an.....................9**

**Uimamu kwao ni nguzo na humkufurisha asiyeamini hivyo...................................................................................12**

**Kumkosea adabu mtumeﷺ, binti zake na Ahlul-Bait.....................................................................................13**

**Kuwakufurisha kwao mama wa waumini Aisha na Hafswa (Allah awaridhie)............................................14**

**Kuvuka kwao mipaka juu ya Ali (Allah amridhie) ..........16**

**Kuvuka kwao juu ya Fatma (Allah amridhie) ................18**

**Kuwatukuza maimamu wao na kuvuka mipaka zaidi ya mitumeﷺ..............................................................................19**

**Kuwakufurisha kwao maswahaba isipokuwa watatu.....21**

**Chuki yao kwa ya Abubakri, Omar na Uthman (Allah amridhie)……………………………………………………………21**

**Mahdi wao wa uwongo na kauli yao kuhusu kurejea……23**

**Kuvuka kwao mipaka katika kuabudu makaburi………..24**

**Kuwapenda kwao makafiri, khiyana zao na kuvunja kwao ahadi……………………………………………………………………25**

**Chuki yao dhidi ya Makka na Madina………………………27**

**Chuki yao dhidi ya Misri na Sham……………………………27**

**Kula watu wa vilemba miongoni mwao khumus…………21**

**Kujaalia kwao kujipiga makofi na kurukaruka ni ibada kubwa ya kujikaribisha "kwa Husein"………………………21**

**Kuhimiza kwao juu ya mutaa' pamoja na kufanya mutaa' na wanawake wazinifu………………………………………………21**

**Taqiyya na uwongo ni msingi wa madhehebu yao………22**

**Kuwakufurisha kwao waislamu na chuki yao dhidi yao 23**

**Chuki yao kwa ahlu sunnah ni kubwa zaidi ya wasifu…24**

**Khuraafaat "mambo ya uwongo" ya ki-shia………………25**
**Vitabu muhimu katika kuwajibu Shia Ithnaasharia…….27**

**Tovuti muhimu "za internet" katika kuwajibu shia ithnaasharia……………………………………………………………28**

## Utangulizi

Sifa njema zote anastahiki Allah, na swala na salamu zimfikie mjumbe wake, maswahaba, taabi'na, na kila ataefuata muongozo wake.

Huu ni muendelezo mfupi katika kuwabainishia waislamu itikadi za makundi potofu, ili wajihadhari; na hasa baada ya kuwa zimenyanyuka sauti za wengi miongoni mwao katika masiku haya, na kupata nguvu ya kueneza batili zao.

Tumeanza na kundi la (Shia Ithnaashariyya) baina ya makundi mengi ya kishia; sababu ndilo kundi lenye wafuasi (wengi) wanaopatikana nchini Iran, Iraq na nchi za Ghuba…

Kama kawaida kundi hili linakithirisha kudai kwamba madhehebu yao hayatofautiani na madhehebu ya Ahlus Sunnah, na kwamba wao wamedhulumiwa na kusingiziwa (mambo ya uwongo), na wana juhudi kubwa katika kulinda madhehebu yao pamoja na kueneza vitabu na risala nyingi zenye kulingania kwenye madhehebu hayo, pamoja na kufuatilia vitabu vya Ahlus Sunnah na kujaribu kujibu, kiasi ambacho hakuna mfano wake katika kundi lingine la kishia.

Na wakati ilipokuwa vitabu vya mashia vimekuwa vingi katika zama hizi, na kwa sura ambayo haikuwepo hapo kabla, na kutumia nyenzo mbalimbali katika kuvieneza.

Basi ni wajibu wetu kudhihirisha yale yaliyomo katika itikadi potofu, hata kama wanajitahidi kuzificha.

Kama ilivyosemwa: **(tutaisema dini yenu kutoka kwenye vinywa vyenu)!**

Allah (Subhaanah) ainyanyue bendera ya Ahlus Sunnah pamoja na watu wake, na aiangushe batili na watu wake.

**Abdullahi ibn Muhammad As Salafiy.**

# Utangulizi wa Mfasiri

Kila sifa njema anastahiki Allah Mola wa walimwengu wote, aliyeahidi kukilinda kitabu chake kutoingiliwa na batili wala upotofu wa aina yoyote, kisha swala na salamu zimfikie Mtume wakeﷺ aliyemtuma kwa uongofu na dini ya haki, ili iwe juu ya dini zote hata kama watachukia makafiri.

Kama inavyofahamika ya kwamba Mtumeﷺ aliifundisha dini hii kwa uwazi na utimilifu mpaka akaondoka duniani hali ya kuwa ameuacha Umma wake katika njia iliyo wazi, usiku wake ni sawa na mchana wake, haiepuki njia hiyo ila mwenye kuangamia.

Wakaifuata na kuiandama njia hiyo kwa utimilifu wake na usafi wake maswahaba walio wema (Allah awaridhie).

Ilipofika mwishoni mwa utawala wa makhalifa waongofu (Abubakri, Umar, Uthman na Ali Allah awaridhie) ziliingizwa katika uislamu baadhi ya fikra potofu, ikiwemo fikra ya **myahudi Abdullahi bin Sabai**.

Wakasimama imara watu wema waliotangulia tangu maswahaba pamoja na wale wenye kufuata mwenendo wao (mpaka katika zama hizi) katika kubainisha upotofu na fikra hizo chafu hata ikibidi baadhi yao kuteswa, kufungwa na hata kupoteza roho zao.

Baada ya kuona kasi ya ueneaji wa fikra potofu za myahudi huyo zimegeuzwa kuwa ni dini inayofuatwa na kuenezwa kwa juhudi kubwa na pote la (Shia ithnaasharia/ imaamiyya) kupitia njia mbalimbali, kama vile uchapishaji wa vitabu vilivyotafsriwa kwenye lugha tafauti tafauti ikiwemo Kiswahili, kupia chakula katika vituo vyao na kuwaita watu mbalimbali kuja kula (ili watu wasione ubaya wao), kufungua vituo vya taaluma kwa kuwafundisha watu ima bila kulipia (bure) au kulipa kiasi kidogo ambacho hakifanani na sehemu nyengine mfano wake n.k, na hilo limefanyika katika maeneo mengi

hasa Afrika ya mashariki; ikanilazimu kutoa mchango wangu (pamoja na uchache wa maarifa yangu) katika kutafsiri risala hii:

**( مَــنْ هُــمْ الشِّــيْعَـةُ الْإِثْــنَا عَـشَـــرِيَّــةُ ؟ )**

Kilichoandikwa na Abu Adillahi As Salafy ( حفظه الله ) chenye faida nyingi pamoja na uchache wa kurasa zake, katika kukabiliana na madhehebu haya potofu yenye kudai ati yanawatetea Ahul Bayt ( watu wa nyumbani kwa kwa Mtumeﷺ )!

Mwandishi wa kitabu hiki amejitahidi kutaja kauli na kuegemeza kwenye kitabu husika cha mashia kwa kutaja juzuu na ukurasa ili wasije kusema kwamba wamedhulumiwa (kama wanavyodai).

Allah anasema:

( وَإِذَا قُـلْـتُـمْ فَــاعْـدِلُـوا )

**(Na mnaposema semeni kwa uadilifu)**[1]

**Tanbihi:** hii ni chapa ya pili ya kitabu hiki, chapa ya kwanza ilikuwa (1433h-2012m), kwa kopi takribani (6000).

Katika chapa hii nimejitahidi kurekebisha makosa yaliyojitokeza kwenye chapa ya kwanza, na kuondosha baadhi ya mambo na pia kuongeza yenye kuhitajika ili kukiweka kitabu katika sura nzuri kwa msomaji tafauti na ile ya kwanza.

Alhamdu Lillahi kwa kutimiza dhamira yangu hii kwa mara ya pili, Allah aweke taufiq na qabuli kwa wasomaji, kama ilivyokuwa katika chapa ya kwanza, na awanusuru waislamu na janga la USHIA na kuwaepusha na fikra chafu zinazoenezwa na pote hilo.

WALLAAHU A'LAM

[1]- Surat Al An'aam/152.

## ASILI YA MADHEHEBU YAO

**Miongoni mwa itikadi za shia ithnaasharia:** wao wanakiri na kukubali kwamba ushia asili yake ni **uyahudi** ambao asili yake ni Abdullah ibn Sabai ambae ni myahudi, na kwamba Aliy ibn Abi Twalib (Allah awaridhie) aliwachoma moto na akajietenga nao[2].

Na pia wanakubali na kujifaharisha kwa kuitwa Raafidhwa (wenye kupinga ukhalifa wa Abubakar, Umar na Uthman (Allah awaridhie))[3].

## ITIKADI YAO KWA ALLAH سُبْحَانَهُ وَتَعَالَى

**Wanasema:** "Hakika sisi hatukusanyiki pamoja nao (Ahlus Sunnah) juu ya muabudiwa (mmoja) wala Nabii wala imamu (khalifa), kwa sababu wao wanasema: Muabudiwa wao ni yule ambae mtume wake ni Muhammadﷺ , na khalifa wake baada yake ni Abubakri (Allah awaridhie), na sisi hatumuamini Mola wala Nabii huyo, bali tunasema: Mola ambae khalifa wa mtume wake ni Abubakri (huyo) si Mola wetu, wala Nabii huyo si Nabii wetu[4].

**Na wanasema:** Hakika Allah سُبْحَانَهُ وَتَعَالَى hataonekana siku ya kiama, na wala yeye hasifiwi kwa sehemu, zama, wala haashiriwi, na ataesema kwamba (Allah) anateremka mpaka kwenye mbingu ya dunia, au atadhihiri kwa watu wa peponi kama (unavyodhihiri) mwezi, au mfano wa hayo; basi huyo nafasi yake ni sawa na yule aliyemkufuru[5].

---

[2]- Kitabu: **Firaqus Shiia' (uk: 22)** cha An-Nuubakhti, na **Ikhtiyaaru Maarifati Rrijaal (uk: 107)** cha At-Tuusy.

[3]- Kitabu: **Biharul Anwaar ( j: 65, uk: 97)** cha Al-Majlis.

[4]- Kitabu: **Al-Anwaaru Nnuumaaniyya (j: 2, uk: 278)** cha Al-Jazaairiy.

[5]- Kitabu: **A'qaaidul Imaamiyyah (uk: 58)** cha Muhammad Ridhwa Mudhaffar .

**Na wanasema:** Allah atamshika muumini khaaswira siku ya kiama, na muumini atamshika Mola wake khaaswira, na huku anamkumbusha madhambi yake, ikasemwa: ni vipi huko kumshika khaaswira? Amesema: akaweka mkono wake juu ya kiuno chake (akitafsiri maana ya khaaswira), kisha akasema: kama hivi anavyomzungumzisha mmoja wetu ndugu yake katika jambo ambalo linamfurahisha[6].

**Na wanasema:** Allah وَتَعَالَى anateremka siku ya Arafa mpaka kwenye ardhi wakati linapopinduka jua, akiwa juu ya ngamia ambae kwato (miguu) yake iko mbalimbali, huku akiwarukia watu waliopo katika viwanja vya Arafa upande wa kulia na kushoto[7].

**Na wanasema:** Hakika kulielekea kaburi ni jambo la lazima, hata kama haliko (upande wa) kibla, kwani kulielekea kaburi kwa anaezuru (makaburi ya wakubwa wa kishia) ni sawa na kuelekea kibla nalo ni (wajhullahi); yaani upande wake ambao ameamrisha watu waelekee katika hali hiyo[8].

**Na wanasema:** Neno (آهْ: Aah) ni jina miongoni mwa majina ya Allah yaliyo mazuri, ataetamka hivyo basi amemtaka msaada Allah[9].

**Na wanasema:** Allah anamtembelea Husein bin Ali (Allah awaridhie) na anampa mkono, na kukaa pamoja nae juu ya kitanda[10].

---

6- Kitabu: **Al-Usuulus Sittatu A'shar (uk: 203),** kwa uhakiki wa: Dhiyaauddiin Mahmudy

7- Kitabu: **Al Usuulus Sittatu Ashar (uk: 204),** kwa uhakiki wa: Dhiyaauddiin Mahmudy

8- Kitabu: **Bihaarul Anwaari ( j: 101, uk: 369)** cha Al-Majlis.

9- Kitabu: **Mustadraqul Wasaail ( j: 2, uk: 148)** cha An-Nuuri Ttwabrasy.

10- Kitabu: **Swahiifatul Abraari ( j: 2, uk: 140)** cha Mirza Taqiy**.**

## KAULI YAO JUU YA KUPOTOSHWA QUR'AN

**Na wanasema (na kukubali):** juu ya kupotoshwa kwa Qur'an tukufu na kupunguzwa, na kwamba Qur'an sahihi anayo Mahdi wao aliyejificha (pangoni).

Na miongoni mwa maulamaa wakubwa wa shia imaamiyya waliosema juu ya kupotoshwa Qur'an ni**:**

1- Ali ibn Ibrahim Al Qummi.
2- Ni'matullahi Al Jazaairiy.
3- Al Faidhwul Kaashaany.
4- Ahmad At Twabrasi.
5- Muhammad Baaqir Al Majlis.
6- Muhammad ibn Nu'man.
7- Abul Hasan Al Aa'miliy.
8- Adnaan Al Bahraaniy.
6- Yusuf Al-Bahraaniy.
7- An Nuur At Twabrasi.
11- Habiibullahil Khuuiy.
12- Muhammad ibn Ya'qub Al kuleyni
13- Muhammad Al-A'yyash. Na wengine[11].

**Na wanasema:** Neno Aali Muhammad na Aali Aliy limeondoshwa ndani ya Qur'an[12].

**Na wanasema:** Hakika hakuna waliokusanya Qur'an isipokuwa maimamu (wa kishia), nao wanaijua elimu yake yote[13].

---

[11]- Kitabu: **As Shiiatu Ithnaasharia watahriiful Qur'an** cha Muhammad seif, na **Mauqifu Rraafidhwa Minal Qur'anil karim** cha kaaram'biiry.

[12]- Kitabu: **Minhaajul Baraa' Sharhu Nahjil Balaagha ( j: 2, uk: 216)** cha Habibullahi Al Khuuiy.

[13]- Kitabu: **Usuulu Kaafi ( j: 1, uk: 228)** cha Al Kuleyn.

**Na wanasema:** Qur-an si hoja isipokuwa kwa yule aliye na msimamo[14].

**Na wanasema:** Kuna sura inaitwa **Al-wilaya,** na wanadai kwamba Uthman ibn Affan (Allah amridhie) ameifuta (ndani ya msahafu)[15], aya ya kwanza (inasema)

**(يآيها الذين آمنوا آمنوا بالنورين)**
(Enyi mlioamini aminini nuru mbili).

**Na wanasema:** (Ati) kuna msahafu unaitwa msahafu wa Fatma (Allah amridhie) , yaliyomo ndani yake ni mfano wa Qur'an yetu hii mara tatu[16].

**Na wanasema:** Huku wakibadilisha maana katika aya ya Allah inayosema:

( يَاأَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ )

**(Ewe Nabii fikisha yale yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa mola wako na kama haukufanya basi utakuwa haujafikisha ujumbe wake)[17]..**

(Shia ithnaasharia) wamesema:

( بَلِّغْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ - فِيْ عَلِيٍّ- وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ )

(Fikisha yale yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa mola –**kuhusu (ukhalifa wa) Aliy-** na kama haukufanya basi utakuwa haujafikisha ujumbe wake).

Wakazidisha kwa madai yao neno: (فِيْ عَلِيٍّ)!

---

14- Kitabu: **Usuulul Kaafi ( j: 1, uk: 169)** cha Kuleyn.

15- Kitabu: **Faslul khitwaabi fii tahriif kitabi Rabbil Arbaab (uk: 18)** cha At Twabrasi.

16- Kitabu: **Usuulul Kaafi ( j: I, uk: 239)** cha Al kuleyni.

17- Surat Al Maida/67.

Maana yake ni kwamba Mtume ﷺ amesahau, kwa maana ameacha, na huenda aliogopa wanafiki (isije wakamdhuru Aliy Allah amridhie) kama alivyosema hayo (mtume ﷺ ) katika maneno yake mengi[18], (wanafiki wanaokusudiwa hapa ni maswahaba wakiongozwa na Abubakri, Umar na Uthman (Allah amridhie).

**Na wanasema:** Hawampingi yule anaesema juu ya kupotoshwa kwa Qur'an (At Thaqlul Akbar), bali wanamzingatia kuwa ni Mujtahid, ama yule anaepinga ukhalifa kwa Aliy (At Thaqlul Aswghar) huyo kwa mashia ni kafiri, wala hakuna shaka juu ya ukafiri wake[19].

**Na wanasema:** Wao wamewaamrisha wafuasi wao kuisoma Qur'an hii iliyopo (mikononi mwetu) ndani ya swala na sehemu nyengine, na kufanyia kazi hukumu zake, mpaka atapodhihiri bwana wa zama (Al Mahdi) halafu iondoshwe Qur'an hii mikononi mwa watu na iende mbinguni, kisha itoke Qur'an ambayo ameitunga Amirul Muuminina (Ali ibn Abi Twalib Allah amridhie) kisha isomwe pamoja na kufanyiwa kazi hukumu zake[20].

**Na wanasema:** Msiwafundishe wake zenu surat Yusuf wala (nyinyi) msiisome mbele yao; kwa sababu ndani yake kuna fitna, bali wafundisheni surat An Nnur kwa sababu ndani yake kuna mawaidha[21].

## UIMAMU KWAO NI NGUZO NA

---

[18]- Kitabu: **Faslul khitwabi fii tahrifi kitab Rabbil Arbaab (uk 182)** cha At Tabrasi

[19]- Kitabu: **Al-I'tiqaadaat (uk: 103)** cha ibn Baabawaihi Al-Qummi.

[20]- Kitabu: **Anwaaru Nnuumaniyya ( j: 2, uk: 363)** cha Ni'matullahi Al Jazaairiy.

[21]- Kitabu: **Al Furuu' Minal Kaafi ( j: 5, uk: 516)** cha Kuleyni.

## HUMKUFURISHA YULE ASIYEAMINI HIVYO

**Na wanasema**: Yule ambae haamini uimamu (wa maimamu 12) haitimii imani yake, mpaka akiamini na kuitikadi hivyo[22].

**Na wanasema:** Hakika uimamu ni muendelezo wa utume, na dalili yenye kuwajibisha kupelekwa mitume na manabii basi hiyohiyo ndio dalili yenye kuwajibisha kusimamisha uimamu baada ya mtume[23].

**Na wanasema:** Makusudio yao kuhusu uimamu ni: cheo cha Allah, yeye ndie anaechagua kwa kile kilichotangulia katika elimu yake juu ya waja, kama vile anavyomchagua mtume na kumuamrisha (aujulishe umma kuhusu uimamu)[24], na awaamrishe wafuasi wake kumfuata (imamu huyo)[25]. Bali uimamu ni msingi katika misingi ya dini, haitimii imani isipokuwa kwa kuitakidi hivyo, na pia wanasema: Uimamu ni muendelezo wa Utume.

**Na wanasema:** Hakika mwenye kupinga uimamu wa Amirul Muuminina Ali ibn Abi Twalib (Allah amridhie) na maimamu (waliokuja) baada yake ni kama aliyepinga utume, na yule atemkubali Amirul Muuminina na akamkataa mmoja kati ya wale waliokuja baada yake miongoni mwa maimamu, basi huyo ni sawa na yule aliyewakubali mitume wote, halafu akakanusha utume wa Muhammad ﷺ. **Na wanasema:** Ataepinga uimamu wa mmoja kati yao huyo ni sawa na mtu aliyekanusha mitume wote[26].

---

22- **A'qaaidul imaamiyya (uk: 78)** cha Muhammad Ridhwa Mudhwaffar.

23- **A'qaaidul imaamiyya (uk: 88)** cha Muhammad Ridhwa Mudhwaffar.

24- **Kwa maana kila mtume aliamrishwa autangaze ukhalifa wa Ali.**

25- **Aslu Shia Wausuuluha (uk: 102)** cha Muhammad Kaashiful Ghitwaa.

26- **Minhaju Nnajaat (uk: 48)** cha Faidhul Kaashany.

**Na wanasema:** Wamekubaliana **Shia imaamiyyah** kwamba ataekanusha uimamu wa mmoja kati ya maimamu (kumi na mbili 12), na akapinga yale aliyowajibisha Allah mtukufu katika ulazima wa kuwatii, basi huyo ni kafiri, mpotevu, mwenye kustahiki kukaa motoni milele[27].

**Na wanasema:** kuachiliwa neno la shirki na kufru kwa mtu asiyeitikadi uimamu wa Amirul Muuminin na maimamu miongoni mwa watoto wake na akamfadhilisha mwengine juu yao inajulisha kwamba hao (wenye kuwapinga maimamu) ni wenye kukaa motoni milele[28].

## KUMKOSEA ADABU MTUME ﷺ NA BINTI ZAKE PAMOJA NA AHLUL BAYT

**Na wanasema:** Mtumeﷺ wakati alipozaliwa alikaa baadhi ya masiku hana maziwa Abu Twalib (Ami yake) akamrusha (mtumeﷺ ) katika chuchu zake, halafu Allah akateremsha ndani yake maziwa, akanyonya kwake baadhi ya siku mpaka Abu Twalib alipompata (mjakazi) Halima As Saadiyya akamkabidhi[29].

**Na wanasema:** Aliy (Allah amridhie) ni shujaa kuliko Mtumeﷺ , bali yeye (Mtumeﷺ) wala hakupewa ushujaa kabisa[30].

**Na wanaosema:** Mtumeﷺ alikuwa halali mpaka abusu mashavu ya Fatma(Allah amridhie) au (anabusu) baina ya matiti yake[31].

---

27- **Haqqul yaqin fii ma'rifat usuliddin ( j: 2, uk: 179)**, Abdullah Shabri

28- Kitabu: **Biharul Anwaar ( j: 23, uk: 390)** cha Al Majlis.

29- Kitabu: **Usuulul Kaafi ( j: 1, uk: 448)** cha Al Kuleyni.

30- Kitabu: **Al Anwaaru Nnu'maniyya ( j1, uk 17)** cha Ni'matullahi Al Jazairiy.

31- Kitabu: **BihAarul Anwaar ( j 42, uk 43)** cha Al Majlis.

**Na wanasema:** Mtume ﷺ hana mtoto wa kike zaidi ya Fatma (Allah amridhie), ama Ruqaiya, Zainabu na Ummu Kulthum (Allah amridhie) ni (watoto) wa kulea tu[32].

**Na wanasema:** Husein ibn Aliy (Allah awaridhie) amewadhalilisha waumini, kwa sababu yeye amempa baia (kiapo cha utiifu) Muaawiya (Allah amridhie) [33].

## KUMKUFURISHA KWAO MAMA WA WAUMINI AISHA NA HAFSA (ALLAH AWARIDHIE)

**Na wanasema:** Inawezekana mke wa mtume kuwa kafiri, kama mke wa Nabii Nuhu na Nabii Lut (Alayhima Sswalaat was Salaam)**,** makusudio ya mke wa Mtume (hapo) ni mama wa waumini Aisha (Allah amridhie) (Allah amridhie yeye na baba yake)[34].

**Na wanasema:** Aisha (Allah amridhie) baada ya kufa Mtume ﷺ aliritadi kama walivyoritadi kundi kubwa miongoni mwa maswahaba[35].

**Na wanasema:** Aisha (Allah awaridhie) amekusanya dinari arobaini za uzinifu, na akawagawia watu wanaomchukia Ali (Allah amridhie)[36].

**Na wanasema:** Mama wa waumini Aisha (Allah amridhie) alifanya uzinifu, (Allah atulinde) na katika kauli ya Allah inayosema:

---

[32]- Kitabu: **Daairatul Maarifil Islamiyya Sshii'yya ( j 1, uk 27)**.

[33]- Kitabu: **Rijaalul Kasshi (uk 103)** cha Al Kasshi.

[34]- Kitabu: **Hadithul Ifki (uk 17)** cha Jaafar Murtadhwa.

[35]- Kitabu: **As shihaabu Tthaqib fii bayaani Ma'na Nnaaswib (uk: 237)** cha Yusuf Al Bahraany.

[36]- Kitabu: **Mashaariq Anwaaril Yaqin (uk: 86)** cha Rajab Al Barsi.

( أُولَئِكَ مُبَرَّءُونَ مِمَّا يَقُولُونَ )

"Hao wameepushwa na hayo wanayoyasema"

**Mashia wanasema:** Maana ya aya hii ni kumtakasa Mtume wake ﷺ na uzinifu, wala si Aisha[37].

**Na wanasema:** Hafswa (Allah awaridhie) amekufuru, kwa kusema:

( مَنْ أَنْبَأَكَ هَذَا)

**"Nani aliyekupa habari hii?"[38].**

Na Allah akasema kuhusu (Hafswa) na Aisha:

( إِنْ تَتُوبَا إِلَى اللَّهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوبُكُمَا )

"Kama nyinyi mtatubia kwa Allah (basi inataka mfanye upesi upesi) kwani nyoyo zenu zimemili upande kidogo"[39].

**Wanasema:** neno (صَغَتْ) lina maana ya: ( زَاغَبْ ), nayo ni ukafiri.

**Na (wanasema):** wameshirikiana kumnywesha Mtume ﷺ sumu, na Allah alipompa habari juu ya kitendo chao hicho alitaka kuwauwa, (lakini) wakaapa ya kwamba wao hawakufanya, basi Allah akateremsha aya:

( يَاأَيُّهَا الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَعْتَذِرُوا الْيَوْمَ )

**(Enyi mliokufuru msilete udhuru leo[40])[41].**

---

37- **As Swiratul Mustaqim ( j: 3, uk: 165)** cha Zainuddin An Nnabaatwi.

38- Surat At Tahriim/3.

39- Surat At Tahriim/4.

40- Surat At Tahriim/7.

41- **As-swiratul mustaqim ( j: 3, uk: 168)** cha Zainuddin An Nnabatwiy.

## KUVUKA KWAO MIPAKA JUU YA ALI رَضِيَ اللهُ عَنْهُ

**Na wanasema:** Allah amemsemesha Mtumeﷺ katika siku ya miraji kwa sauti na lugha ya Ali ibn Abi Twalib (Allah amridhie) [42].

**Na wanasema:** Allah alimnong'oneza Ali ibn Twalib (Allah amridhie) katika sehemu ya Twaif, na alikuwepo baina yao Jibril[43].

**Na wanasema:** Ali Ibn Abii Twalib (Allah amridhie) ndiye mwenye kugawa pepo na moto, atawaingiza watu wa peponi katika pepo, na watu wa motoni katika moto[44].

**Na wanasema:** Allah atamuingiza peponi yule mwenye kumtii Ali (Allah amridhie) hata ikiwa atamuasi Allah, na atamuingiza motoni ataemuasi Ali (Allah amridhie) hata kama atamtii Allah[45].

**Na wanasema:** Ali (Allah amridhie) ndie siri ya mitume, na Allah amesema: Ewe Muhammad, nimempeleka Ali (awe) pamoja na wewe na (kwa) mitume (wengine) katika hali ya kujificha na (awe) pamoja na wewe katika hali ya kudhihiri[46].

**Na wanasema:** Hakika Ali (Allah amridhie) ni hoja kwa Muhammadﷺ , na kwa hakika Muhammadﷺ analingania kwenye ukhalifa wa Ali (Allah amridhie)[47].

**Na wanasema:** Kwa hakika Allah hakupeleka mtume yeyote isipokuwa alilingania juu ya ukhalifa wa Ali (Allah amridhie) kwa hiyari au kwa lazima[48].

---

[42]- **Kashful yaqin fii Fadhwaail Amiril Muuminiin (uk 229)**. Al Huliy

[43]- Kitabu: **Baswaairu Ddarajaat ( j: 8, uk: 230)** cha As Swaffaar.

[44]- Kitabu: **Baswaairu Ddarajaat ( j: 8, uk: 235)** cha As Swaffaar.

[45]- **Kashful Yaqin fii Fadhwaail Amiril Muuminiin (uk: 7)**. Al Huliy

[46]- Kitabu: **Al Asraarul Uluwiyya (uk: 181)** cha Muhammad Al Masoudiy.

[47]- Kitabu: **Baswaairu Ddarajat (uk: 91)** cha Muhammad As Swaffaar.

[48]- Kitabu: **Al Asraarul Uluwiyya (uk 190)** cha Muhammad Al Masoudiy.

**Na wanasema:** Hakika dini haikamiliki isipokuwa kwa ukhalifa wa Amiril Muuminin Ali ibn abi Twalib (Allah amridhie)[49].

**Na wanasema:** Mtume ﷺ amesema: Tambueni hakika Jibril amenijia na akasema: ewe Muhammad ﷺ, mola wako anakuamrisha kumpenda Ali ibn Abii Twalib (Allah amridhie) na (kuupenda) uongozi wake[50].

**Na wanasema:** hakika Ali (Allah amridhie) ataingia peponi kabla ya Mtume ﷺ[51].

**Na wanasema:** Hakika (ukulele wa) radi ni miongoni mwa amri ya swahiba wenu, wakasema: nani swahiba wetu? akajibu: Amirul Muuminina Ali ibn abi Twalib (Allah amridhie)[52], (anakusudia kuwa radi ni sauti ya Ali ).

**Na wanasema:** Hakika Ali ibn Abi Twalib (Allah amridhie) anahuisha wafu, na huleta faraja kwa watu wenye shida[53].

**Na wanasema:** Hatoingia yeyote peponi ila kwa idhini ya Ali (Allah amridhie)[54].

**Na wanasema:** Kuhusu ukafiri wa mwenye kumpinga Ali (Allah amridhie), na kuritadi kwa mwenye kumtukuza mwengine zaidi yake[55].

---

49- Kitabu: **Al Ihtijaj ( j: 1, uk: 57)** cha At Twabrasi.

50- Kitabu: **Baswaairu Ddarajaat (uk: 92)** cha Muhammad As Swaffaar.

51- Kitabu: I'**lalu Sharaai' (uk: 205)** cha ibn Baababawaihi Al Qummi.

52- Kitabu: **Al Ikhtisaas (uk: 327)** cha Al Mufid.

53- Kitabu: **Uyuunul Mu'jizaat (uk: 150)** cha Husein Abdul Wahhab. na risala: **Hilaalul Mushkilaat**.

54- **Manaaqibu Amiril Muuminin (uk: 93)** cha Ali Ibn Maghaaziliy .

55- **Bishaaratul Mustwafaa Lishiiatul Murtadhwaa ( j: 2, uk: 79).**

**Na wanasema:** Hakika Allah amejifaharisha kwa Malaika wake kuhusu Ali (Allah amridhie)[56].

**Na wanasema:** Hakika Mitume na Manabii wametumwa kwenda kuukubali ukhalifa wa Ali ibn Abi Twalib (Allah amridhie)[57]

**Na wanasema:** Hakika Ali ibn Abi Twalib (Allah awaridhie) aliashiria kwa mkono wake juu, mawingu yakasogea na kufanya giza, kisha yakamsalimia, halafu akamwambia Ammar panda na mimi na useme:

( بِسْمِ اللَّهِ مَجْرَاهَا وَمُرْسَاهَا )

**"kwa jina la Allah kuwe kwenda kwake na kusimama kwake"[58]**

Ammar akapanda na wakapotea machoni mwetu[59].

**Na wanasema:** Mbwa aliwauma maswahaba wawili, hiyo ni adhabu ya Ali (Allah amridhie); kwa sababu ya kuwapata wao mori wa ujinga na kibri cha uarabu, na hali ya kuwa mbwa (huyo) alitoa ushuhuda juu ya kwamba Ali (Allah amridhie) ni walii wa Allah, na wasii wa Mtume wake[60].

## KUVUKA KWAO MIPAKA JUU YA FATMA رَضِيَ اللهُ عَنْهَا

**Na wanasema:** Kwamba Fatma, Hasan, Husein (Allah awaridhie) pamoja na familia ya Husein wote hao wamekingwa na kutenda madhambi, isipokuwa (familia) cha Hasan[61].

---

56- Kitabu: **Bisharatul Mustwafaa Lishiiatul Murtadhwaa ( j 1, uk 66)**.

57- Kitabu: **Al Maalimu Zzulfaa (uk: 303) cha Hashim Al Bahraniy**.

58- **Surat Hud/41.**

59- Kitabu: **Bihaarul Anwaar** cha Al Majlis.

60- Kitabu: **Bihaarul Anwaar ( j: 41, uk: 247), na ( j: 17, uk: 30)** cha Al Majlis.

61- Kitabu: **Aqaaidul Imaamiyya (uk: 89 na 98)** cha Al Mudhwaffar.

**Na wanasema:** Kama si Ali (Allah amridhie) asingeumbwa Muhammadﷺ na lau si Fatma (Allah amridhie) msingewaumbwa nyinyi Hasan na Husein)[62].

**Na wanasema:** Fatma (Allah amridhie) ni umbile la kiungu lenye utukufu, limedhihiri katika sura ya kike[63].

**Na wanasema:** Fatma (Allah amridhie) alikuwa anamzungumzisha mama yake wakati yuko tumboni mwake[64].

## KUWATUKUZA MAIMAMU WAO ZAIDI YA MITUME (ALAYHIS SWALAAT WAS SALAAM) NA KUVUKA KWAO MIPAKA

**Na wanasema:** Hakika maimamu wa Shia Ithnaasharia ni bora kuliko Mitume na Manabii (Alayhis Swalaat wa Salaam)[65].

**Na wanasema**: Maimamu wa kishia wanayajua yaliopita na ya wakati wa sasa, hakuna chochote wasichokijua, na hawafi isipokuwa kwa matashi yao[66].

**Na wanaosema:** Maimamu wana cheo cha kusifiwa (Maqaamam Mahmuuda), na daraja ya juu, na tawala za kidunia zinanyenyekea kwao na (kwenye) nguvu yao, na vitu vyote vya dunia (viko chini yao)[67].

---

62- Kitabu: **Al Asraarul Faatwimiyyah (uk: 98)** cha Muhammad Al Masoudiy.

63- Kitabu: **Al Asraarul Faatwimiyyah (uk: 355)** cha Al Masoudiy.

64- Kitabu: **Fatma Zzahraa Minal Mahdi ila Llahdi (uk: 38)**, cha Al Qazwiiniy.

65- Kitabu: **Al Anwaaru Nnu'maaniyya ( j: 3, uk308)**, cha Al Jazairiy.

66- Kitabu: Usulul Kaafi **( j: 1, uk: 258-260)** cha Kulein.

67- Kitabu: **Tahrirul Wasiilah (uk: 52)** cha Khomeini.

**Na wanasema:** Maimamu wa kishia wana utawala ulio kinyume na muumba (Allah), na (utawala wao) ni sawa na utawala wa Allah kwa viumbe[68].

**Na wanasema:** Hakika sisi (maimamu) pamoja na Allah tuna hali nyingi, hawezi kuzifikia Malaika aliye karibu na (Allah) wala Nabii yoyote aliyetumwa[69].

**Na wanasema:** Hakika maimamu kumi na mbili wanaweza kuendesha mambo (ya kilimwengu) kwa idhini yao, na kupitisha qadar, na mfano wa hayo, na hakuna chenye kuwazuia kufanya hivyo, na hilo ni hakika[70].

**Na wanasema:** Hakika maimamu ki-shia hunyanyuliwa na hutolewa katika mapaja wakati wa jimai (tendo la ndoa), wala hawaguswi na uchafu wa manii[71].

**Na wanasema:** Hakika Allah, Malaika, Mitume na waumini wanatembelea kaburi la Amiril Muuminina Ali (Allah amridhie)[72]**.**

**Na wanasema:** Imamu ni sawa na mtume, ni lazima awe amekingwa na kutenda madhambi, uchafu na mabaya yote, yaliyo dhahiri na yaliyojificha, si kwa kukusudia wala kusahau, tangu akiwa mdogo mpaka kufa; kwa sababu wao ni wahafidhina wa sheria, na ni wenye kusimama juu ya mipaka yake, hali yao ni sawa na Mitume[73].

---

[68]- Kitabu: **Miswbaahul Fuqaaha ( j: 5, uk 33)** cha Abul Qasim Al Khuuiy.

[69]- Kitabu: **Tahrirul Wasilah (uk: 94)** cha Khomeini.

[70]- Kitabu: **Al Burhaanul Qaatwii (uk: 14)**, majibu kutokana na maswali ya Aqida na sheria, cha Sheikh wao Muhammad Taqiyyul Bahjat.

[71]- Kitabu: **Madinatul Maajiz ( j: 8, uk: 22)** cha Hashim Al Bahraaniy.

[72]- Kitabu: **Al-Furuul Kaafi ( j: 4, uk: 580)** cha Kuleyn.

[73]- **A'qaaidus Shia ( j: 3, uk: 179)** cha Ibrahimu Az Zinjaaniy.

**Na wanasema:** Hakika Malaika wameumbwa ili kuwatumikia Ahlul Bait[74].

## KUWAKUFURISHA KWAO MASWAHABA WOTE ISIPOKUWA WATATU TU

